East African Journal of Swahili Studies, Volume 7, Issue 1, 2024
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 7, Issue 1, 2024**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mifumo ya Ujinaishaji ya Wameru: Uchunguzi Tarafani Mwimbi katika Jimbo la Tharaka Nithi, Kenya

*Dkt. David Micheni Mutegi, PhD*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Egerton, S. L. P. 536 Egerton, Kenya.
[*] ORCID ID https://orcid.org/0000-0002-3270-664; Barua pepe ya mawasiliano: dmisheni@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*12 Agosti 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Athari, Mbari, Mifumo, Ujinaishaji, na Sifabia.*

## IKISIRI

Lengo la utafiti lilikuwa kubainisha mifumo ya Wameru ya ujinaishaji. Uchunguzi ulifanywa Skatika tarafa ya Mwimbi katika jimbo la Tharaka Nithi nchini Kenya kwa ambavyo hakuna uchunguzi wowote umefanywa kufikia sasa kubainisha namna Wameru wanavyojinaisha watoto. Swali la utafiti katika uchunguzi huu lilikuwa: Wameru huzingatia mifumo gani katika ujinaishaji wa watoto? Majibu kwa swali hili yalibainisha namna Wameru walivyochagua majina waliyowapa watoto. Idadi ya wahojiwa sabini waliteuliwa wakijumlisha vijana hamsini na wazee ishirini kwa kuwa makundi hayo na idadi hiyo ingekuwa kiwakilisho tosha cha wakaazi wa Mwimbi kwa kujibu swali la utafiti na kutosheleza madhumuni yake pia. Mbinu ya mahojiano yenye muundo ilitumiwa ambapo kila mhojiwa aliulizwa swali lile lile lililoulizwa mwingine. Mbinu hii ilifaa utafiti huu kwa vile kila mhojiwa alikuwa na uhuru wa kujieleza kwa hivyo habari nzito na nyepesi ziliweza kupatikana kwa ajili ya kuchuzwa na mtafiti. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi na Matini na hasa zaidi ulizingatia Mtazamo Usemi Kihistoria wa Ruth Wodak. Ilibainika kuwa Wameru huwa na mifumo minne mahsusi ya ujinaishaji mathalani: sifabia za mtoto na za ntaguye, kutumia majina ya Ukoo, majina ya Rika na majina ya Nyoni. Mtafiti alipendekeza wazazi wawashirikishe vijana katika uteuzi wa majina ya watoto ili kuepuka mwelekeo hasi kuhusu majina yao wanapokua. Mapitio ya maandishi yalidhihirisha kuwa uchunguzi wa aina hii haujafanywa katika eneo hili kwa hivyo matokeo yalikuwa ni kichocheo kwa watafiti wengine wa kiisimu ambao wangependa kutafiti kuhusu mifumo ya ujinaishaji ya makabila mengine.

**APA CITATION**

Mutegi, D. M. (2024). Mifumo ya Ujinaishaji ya Wameru: Uchunguzi Tarafani Mwimbi katika Jimbo la Tharaka Nithi, Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 359-370. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100.

**CHICAGO CITATION**

Mutegi, David Micheni. 2024. “Mifumo ya Ujinaishaji ya Wameru: Uchunguzi Tarafani Mwimbi katika Jimbo la Tharaka Nithi, Kenya”. *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 359-370. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

**HARVARD CITATION**

Mutegi, D. M. (2024) “Mifumo ya Ujinaishaji ya Wameru: Uchunguzi Tarafani Mwimbi katika Jimbo la Tharaka Nithi, Kenya”, *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 359-370. doi: 10.37284/jammk.7.1.2100

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

**IEEE CITATION**
D. M. Mutegi "Mifumo ya Ujinaishaji ya Wameru: Uchunguzi Tarafani Mwimbi katika Jimbo la Tharaka Nithi, Kenya", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 359-370, Aug. 2024.

**MLA CITATION**
Mutegi, David Micheni. "Mifumo ya Ujinaishaji ya Wameru: Uchunguzi Tarafani Mwimbi katika Jimbo la Tharaka Nithi, Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Aug. 2024, pp. 359-370, doi:10.37284/jammk.7.1.2100.

## UTANGULIZI

Ni jambo la kawaida kwa kila mja kuwa na jina linalomtambulisha. Tukio la kumpa mtoto jina huwa muhimu sana katika jamii nyingi ulimwenguni. Jina humpa mtoto utambulisho kamili katika jamii. Kulingana na katiba mpya ya Kenya (2010) kipengele cha 13, kuhusu haki za watoto, mtoto ana haki ya kuwa na jina na utaifa pindi tu anapozaliwa. Edward (1996) anadai kuwa majina huwa kumbukumbu ya tabia ya mtu au matendo ya mtu maishani. Greenberg (1980) na Buren (1977) wanadokeza kuwa mwelekeo kuhusu majina huathiri ukubalifu au kutokubalika kwa majina hasa na vijana.

Kwa mujibu wa Berly (2013) ujinaishaji katika jamii za Kiafrika huwa ni tukio la kiubunifu linaloleta muundo wa ukuaji wa kipekee. Waafrika huamini kuwa majina huwa kitu hai na hubeba nguvu ya kuendelea kuishi kutoka kwa Mungu. Jina la mtu huweza kumtofautisha na mwingine na hudhihirisha hulka yake pasipo kujali alivyolipata. Kuelewa dhana iliyosetiriwa katika majina ya Kiafrika huweza kupata uwezo ulio katika jina hilo. Hii ndiyo sababu Waafrika hawafichui jina la mtoto hadi baada ya umri fulani hasa kwa walioshukiwa kuwa na nguvu za kichawi. Waafrika huamini kuwa jina linaweza kuwa la kheri au la shari. Kumpa mtoto jina lisilo sawa huwa ni njia ya kupata laana au bahati mbaya. Aidha, jina la mtu hubadilika kadri anavyopita hatua mbalimbali za maisha kama vile kutoka utotoni hadi utu uzima au kutoka hadhi ya chini hadi ya juu.

Kulingana na Laura (2009) jamii ya Wameru kama zilivyo jamii nyingi za Kiafrika, hutambulika kwa utamaduni wake wenye miviga mingi mathalani mviga wa ndoa, tohara, mazishi na hasa zaidi mviga wa kumpa mtoto jina. Kwa Wameru majina na miviga inayohusu ujinaishaji huwa muhimu sana katika maisha ya mwanadamu. Ujinaishaji ni desturi iliyoendelea maishani kama vile baada ya kupashwa tohara ambapo baba angemchagulia mvulana jina naye mama akamchagulia msichana. Wameru huwa na mfumo wa kipekee unaotofautisha majina ya kike na ya kiume katika kiwango cha mofolojia, semantiki na pragmatiki ambapo ya kiume na ya kike huwa na viambishi awali tofauti na huwa na maana tofauti kulingana na jinsia.

Pamela na Linda (2014) wanadai kuwa mtoto anastahili kupewa jina litakalomfaa utotoni na katika utu uzima bila kuibua jina la lakabu au la bandia litakalomfedhehesha. Wanasema kuwa jina lina uwezo wa kumfanya mtoto awe na ustahifu wa kibinafsi na vilevile kutambulika. Kulingana nao, kuchagua jina huwa ni jukumu nyeti kuliko kuzaa kwa vile mtu hufanya uamuzi wa kudumu. Greg (2014) ana maoni sawa na haya kwa kudai kuwa jina hueleza mtu alivyo na ni kitambulisho cha mtu atakavyotazamwa na kutendewa na wengine.

Ujinaishaji ni tukio muhimu ambalo huenziwa na wanajamii wote kwa hivyo jina halichaguliwi hivi hivi bali kuna utaratibu na vigezo ambavyo huzingatiwa kwa kufuata ruwaza fulani. Beidelman (1974) anadai kuwa kuna maelezo machache kuhusu mfumo wa ujinaishaji hasa katika Afrika mashariki. Kwa mintarafu hii mfumo wa ujinaishaji ni kipengele muhimu katika utafiti wa kiisimu hasa katika lugha za Kiafrika ambazo utafiti wa aina hii haujafanywa kwa kina.

### Suala la utafiti

Dhima kuu ya jina ni kumtambulisha mtu kibinafsi. Wameru huwa na mfumo wa kipekee wa ujinaishaji wenye taratibu za kuegemeza majina kuumeni na unaotambulisha jinsia kutokana na viambishi awali vya majina. Hata hivyo kadri tujuavyo, hakuna utafiti wowote umewahi kufanywa kufikia sasa kubainisha wazi

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

mifumo ya ujinaishaji ya Wameru. Utafiti huu kwa hivyo ulichunguza mifumo mbalimbali ya ujinaishaji ya Wameru, mfano wa Tarafa ya Mwimbi katika jimbo la Tharaka Nithi nchini Kenya.

**Lengo la utafiti**

Lengo la utafiti huu lilikuwa: kubainisha mifumo ya ujinaishaji ya Wameru

**Madhumuni ya utafiti**

Madhumuni ya utafiti yalikuwa: Kuchunguza mifumo ya ujinaishaji ya Wameru.

**Swali la utafiti**

Wameru huzingatia mifumo gani katika ujinaishaji wa watoto?

## UHAKIKI WA MAANDISHI

### Mfumo wa kujinaisha kulingana na utangamano na mahusiano ya kijamii

Barnes (1980) anadai kuwa kuna sheria zinazozingatiwa katika ujinaishaji kulingana na utangamano na mahusiano ya kijamii. Anatoa mfano wa jamii zingine za Marekani kama Hidasta na Omaha ambao hutumia mfumo wa kuchagua majina ya vitu vionekanavyo na visivyoonekana kama vile: majina ya rangi, visu, vyuma, kimbunga, wanyama, makazi, sauti za ng'ombe na thamani za kibinafsi kama hekima, shughuli za upishi na mafanikio kama vile ushindi.

### Mfumo wa kutumia muundo nyuma wa majina

Buren (1977) alishughulikia muundo wa majina ya kike ambayo hubuniwa kwa kutumia mbinu ya muundo nyuma. Kwa mfano, majina kama Beck kutokana na Becky, Pen kutokana na Penny au Deb kutokana na Debbie. Uundaji huu hudhihirisha uchangamfu mwema wa kibinafsi na uhusiano maalum katika mahusiano ya kawaida ya watu wanaojitambulisha. Kwa kutumia muundo huu wa -ie- *au* -y- huonekana kama wenye dhana ya kitoto na kwa hivyo hutumia muundo maalum kama uhusiano wao ulivyo maalum. Kwa mfano, katika shule za upili wasichana wanaweza kuita rafiki zao kama vile Lydia - Lyd , Jackie -jaq, Alison -Al na Debbie – Deb. Walimu wao hawawezi kuwaita hivi kwani uhusiano wao ni tofauti.

Wierzibickar (1992) anaeleza mifumo ya ujinaishaji ya Kimarekani, Kipoli na Kirusi. Alishughulikia kwa kina miundo ya majina ya kike na ya kiume. Aidha, ameyagawa katika kategoria za majina yagawikayo na yasiyogawika. Mtazamo wake ulilenga sana kuonyesha aina za majina na tofauti za kimuundo huku akiacha pengo la kisemantiki kuhusu majina hayo. Vile vile hakutathmini mielekeo ya watu kuhusu majina waliyotambuliwa kwayo.

### Mfumo wa kujinaisha kulingana na hali au majaaliwa ya mtoto.

Kulingana na Abena (2010) jamii za Kiafrika kama vile Waghana na Wanigeria walikuwa na mfumo wa kuwaita ndugu wawili jina moja. Hali hii ilichangiwa na mambo kama vile: kuzaliwa na kufa kwa mtoto mchanga ambapo ambaye angezaliwa baadaye angepewa jina lile lile. Mtoto wa mke wa pili angepewa jina sawa na wa mke wa kwanza. Jamii ya *Gao* wangeita watoto mapacha jina sawa lakini moja lilifupishwa mathalani, Oko-Akuele, Akwate-Akuate. Berly (2013) anadokeza kuwa jamii za Kiafrika zilitumia ruwaza tofauti tofauti katika ujinaishaji. Wasudani walimpa mtoto jina kutegemea hali ya kuzaliwa kwake kama vile aliyezaliwa afyani aliitwa *Nyawela* naye kifungua mimba akaitwa *Kongel*. Maelezo sawa na haya yanatolewa na Mbiti (1992), anapodai kuwa iwapo watoto walizaliwa wakifa aliyesalia alipewa jina la mnyama au jina lisilopendeza kama njia ya kuonyesha kuwa wazazi wake walikata matumaini yake ya kuishi na vilevile kuficha utambulisho wao ili wasije wakachukuliwa na mizimu. Kwa mfano, Wakikuyu na Waembu walimwita mvulana *Ngari* yaani Chui au Njogu – Tembo. Wameru waliita mvulana Iguna na msichana Kaguna kumaanisha Nyani na vilevile walitumia jina Mati (majani makavu). Waluyia humwita mvulana makokha (takataka).

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

**Mfumo wa kujinaisha kutegemea majira na nyakati za uzazi**

Kulingana na Idowu (1991) baadhi ya makabila ya Kiafrika yalikuwa na mfumo wa kujinaisha kwa kutumia majina ya siku za Juma. Anatoa mfano wa Waswahili wa Afrika Mashariki waliotumia majina kama : Mwajuma kumaanisha alizaliwa siku ya Ijumaa, Esi alizaliwa siku ya Jumapili, Khamisi- alizaliwa siku ya Alhamisi, Jumaane - aliyezaliwa siku ya Jumanne. Jamii ya Yoruba wa Afrika magharibi walikuwa na majina kama Bosede lililomaanisha kuwa alizaliwa siku ya Jumapili. Utaratibu mwingine uliotumiwa ulikuwa wa kutumia orodha ya kuzaliwa. Makabila yaliyotumia mfano huu ni kama vile Waakhani wa Ghana na Waswahili wa Afrika mashariki. Kwa mfano, Nkruma kwa Waghana lilimaanisha alizaliwa akiwa wa tisa katika familia nalo Nsia alikuwa wa sita. Waswahili walitumia majina kama Mosi - alizaliwa akiwa wa kwanza. Waafrika wengine waliotumia majina ya siku za juma na majina ya kidini yaliyomrejelea Mungu ni Wamisiri, Wachaga na Waswahili. Berly (2013), ana maoni sawa na haya kwa kudai kuwa jina Rabhai lilimaanisha aliyeleta mvua.

Idowu (1991) Mbiti (1992) wanafafanua zaidi ruwaza za ujinaishaji katika makabila ya Kenya kama vile, Waluo, Wakalenjin, Waluyia, Wakikuyu na Wameru. Wanadokeza kuwa hali ya anga na majira wakati wa kuzaliwa kama vile gharika, ukame, njaa, wakati wa kuvuna na kupanda, nyakati za siku na matukio makuu ya kihistoria zilichangia upataji wa majina. Aliyezaliwa wakati wa mvua: Waluo walitumia jina Okoth (mvulana) na Akoth (msichana). Wakikuyu waliwaita Kiambura (mvulana) na Nyambura / Kabura (msichana). Wakamba waliwaita Wambu*a* (mvulana) Syombua (msichana). Wakalenjin waliwaita Kiprop (mvulana) Cherop (msichana).Wameru waliita msichana *Kambura*. Waliozaliwa wakati wa kuvuna: Waluyiah waliwaita Wekesa (mvulana) na Nekesa msichana. Vilevile wakati wa kupanda waliita msichana Nakhumicha. Umuhimu wa matumizi ya majina haya ulikuwa kuweka kumbukumbu ya matukio haya na vilevile kukumbusha wakati mtoto alizaliwa kwa sababu hakukuwa na rekodi ya maandishi au njia nyingine ya kuhifadhi historia.

**Msingi wa nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi hakiki usemi na hasa ulizingatia mtazamo usemi kihistoria. Kwa mujibu wa Wodak (2001*)* nadharia ya uchanganuzi hakiki usemi iliasisiwa na maprofesa watambulika wa isimu tekelezi katika bara Uropa kama vile Ruth Wodak, Norman Fairclough na Van Dijk. Lengo kuu la nadharia hii ni kuchambua matini kwa kina kwa minajili ya kuleta uangavu. Huangazia matini ambacho ndicho kipashio chake cha kimsingi kwa kulishughulikia suala la kutokuwa na usawa katika uhusiano. Vilevile huzingatia masuala ya kimukhtadha kwa minajili ya kutoa mahitimisho ambayo yana uangavu zaidi. Nadharia hii ina mihimili mitano lakini mitatu ndiyo ilifaa utafiti huu.

Mhimili wa unominishaji au urejeaji. Fairclough (1995) Anaeleza kuwa nguzo hii inahusiana na suala la jinsi watu huwabandika wengine sifa na hulka mbalimbali na katika mikhtadha gani? Watu huwabandika wengine majina kutokana na sifa zao za kimaumbile au kitabia. Sifa hizi zinaweza kuwa nzuri au mbaya. Mhimili huu ulisaidia mtafiti kugundua sifa zilizotumika kuwapa watu majina.

Mhimili wa mkabala. Nguzo hii hujibu swali kama, watu huwabandika wengine sifa katika mkabala gani? Mkabala ungeweza kuwa wa kikabila, kudunisha au wa kupendelea. Katika ujinaishaji watu hubandika wengine sifa na majina kwa kuongozwa na mikabala mbalimbali. Kutokana na mhimili huu mtafiti alibaini mielekeo ya watu kuhusu majina waliyowapa wengine hasa watoto.

Mhimili wa kudhihirisha nguvu za usemi. Fairclough (1995) anadai kuwa nguzo hii inahusu kujibu maswali yanayohusiana na matamshi katika usemi, je, matamshi huwa ni ya moja kwa moja au kama yaliyogubikwa kiasi gani? Mhimli huu ilimfaa mtafiti katika kuchunguza vipengele

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

vilivyoongoza uteuzi wa majina yaliyopewa watoto na maana ya majina hayo.

## MBINU ZA UTAFITI

### Muundo wa utafiti.

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo ili kubainisha mifumo ya ujinaishaji ya Wameru. Muundo huu ulifaa kwa kuwa utafiti ulihusu kukusanya maoni na sababu za watu kupewa majina ya pekee na kueleza maana na asili ya majina hayo. Muundo wa kimaelezo pia ulifaa kwa vile unaruhusu matumizi ya mahojiano ya ana kwa ana kama njia ya kukusanya deta ambayo ni mbinu iliyotumiwa katika utafiti huu. Kulingana na Orodho (2003), muundo wa utafiti wa kimaelezo ni mbinu ya kukusanya habari kwa njia ya kuhoji sampuli ndogo ambayo ndiyo mbinu iliyotumiwa katika utafiti huu kwa kuwahoji vijana na wazee katika makundi madogo. Mugenda na Mugenda (1999), wanadai muundo wa kimaelezo ndio labda mbinu nzuri inayoweza kutumiwa na wanaisimu jamii wanaopenda kukusanya deta halisi. Maoni haya yanaafikiana na utafiti huu kwa ambavyo ni wa kiisimu jamii uliodhamiria kupata deta halisi kuhusu mifumo ya ujinaishaji na maana ya majina ya wameru kupitia mahojiano ya ana kwa ana. Utafiti huu ulikuwa wa kithamano kwa hivyo matokeo yake yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo.

### Mahali pa utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika tarafa ya Mwimbi Jimboni Tharaka Nithi, Kenya

### Kundi lengwa

Kundi lengwa katika utafiti huu lilikuwa wakaazi wote wa Mwimbi: wazee kwa vijana wa tarafa ya Mwimbi katika jimbo la Tharaka Nithi. Kundi hili liliteuliwa kwa ambavyo liliwakilisha jamii nzima ya Meru kama inavyojihusisha katika ujinaishaji wa watoto.

### Uteuzi wa sampuli.

Utafiti huu ulilenga wazee wa Mwimbi wa jinsia zote. Uteuzi wa sampuli ulikuwa wa kimakusudi ili kuteua vijana hamsini kutoka katika shule tano za upili katika maeneo mbalimbali ya tarafa hii. Wazee ishirini pia waliteuliwa wenye umri wa kati ya miaka sabini au zaidi ambao walitoka sehemu mbalimbali kwa kuzingatia pia usawa wa jinsia: wanaume kumi na wanawake kumi. Uteuzi huu wa sampuli kutoka maeneo mbalimbali na usawa wa jinsia ulihakikisha deta ambayo ilipatikana ilikuwa jumuishi kwa kuwakilisha Wameru wote. Kulingana na Onyango (2001) ukubwa wa sampuli unaolingana na ukubwa ukubalikao katika utafiti wa kimaelezo huwa ni wa asilimia 10 - 20 ya watu wote wa eneo la utafiti. Hata hivyo kulingana na Onyango, sampuli kubwa ni bora iwapo kundi lengwa ni kubwa. Mugenda na Mugenda (2003), wanafafanua kuwa mbinu hii ya uteuzi wa sampuli kimakusudi huwezesha mtafiti kutumia mifumo iliyo na habari itakikanayo kuhusiana na madhumuni ya utafiti.

Kulingana na Kombo na Orodho (2002), istlahi muundo wa utafiti humaanisha mpango wa sehemu ya utafiti unaoonyesha namna mifano itakavyochaguliwa kwa ajili ya uchunguzi. Webber, (1987) anafafanua zaidi kuwa sampuli ni sehemu ndogo ya takwimu ya idadi ya watu ambao hali zao zinachunguzwa ili kuielewa yote. Kwa mintarafu hii sampuli ndogo ya wazee 50 na vijana 20 iliteuliwa ili kuwakilisha jamii ya Wameru kuhusiana na mada iliyochunguzwa. Vijana walishirikishwa ili kuchunguza iwapo walielewa mifumo ya ujinaishaji maadamu wao pia ni sehemu ya jamii. Jumla ya majina 80 yalichaguliwa kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya ujinaishaji. Majina haya yalichaguliwa kwa msingi kuwa ndiyo yalitumika sana kujinaisha wototo na watu wazima. Vilevile yaliwakilisha ruwaza mbalimbali za ujinaishaji wa Wameru.

### Njia za ukusanyaji wa deta

Kuna masuala ya kiutaratibu yaliyoshughulikiwa kabla ya kwenda nyanjani kukusanya deta.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

Kwanza mtafiti alipata kibali kutoka Chuoni Kikuu cha Egerton ili kumhidhinisha kufanya utafiti, kupata kibali kutoka kwa walimu wakuu wa shule za upili ambazo sampuli ya vijana ilipatikana kwani njia ya mahojiano. Kutembelea wazee mastakimuni mwao ili kuwaomba kuwa na kikao nao kwa ajili ya mahojiano na kupanga siku na wakati. Mtafiti pia aliandaa maswali ya mahojiano kwa wazee na vijana ili kuepuka kujirudia au kupoteza wakati kwa kuuliza na kuelezwa mambo yasiyohusiana na madhumuni ya utafiti. Vifaa vingine vya kukusanyia deta vilikuwa video na kitabu cha nyanjani. Kulingana na Abagi (1995), vifaa hivi vilifaa kwa sababu hakuna habari ingeweza kupotea, kusahaulika au kuvurugwa iwapo ingehifadhiwa katika vifaa hivyo. Mtafiti alitumia mahojiano ya ana kwa ana katika kukusanya data kwa vile mbinu hii iliufaa uchunguzi huu kwa ambavyo hukusanya habari iliyo wazi, yakini na ya kutegemeka kutoka kwa wahojiwa. Habari hiyo ilihusu hisia, mielekeo na uzoefu wa kibinafsi kuhusu, mifumo ya ujinaishaji katika jamii. Mahojiano pia yalifanyika vyema kwa vile sampuli iliyokusanywa ilikuwa ndogo. Mtafiti vilevile alitumia video na kitabu cha nyanjani kurekodi majibu ya wahojiwa kwa ajili ya uchanganuzi wa deta wa baadaye.

### Uchanganuzi wa deta

Deta iliyopatikana kutokana na mahojiano ya ana kwa ana ilichaguliwa kulingana na madhumuni na masuala ya utafiti. Mbinu ya maelezo ilitumiwa kuchanganua deta na baadaye kuripotiwa kwa kutumia majedwali machache kwa kuwa ulikuwa uchunguzi wa kithamano usiohitaji hesabu. Mtafiti pia alifanya muhtasari wa matokeo baada ya kupitia deta iliyokusanywa na kutambua ujumbe muhimu kulingana na mada ya utafiti.

## UWASHIRISHAJI NA UCHANGANUZI WA DETA

### Ujinaishaji kutokana na sifabia za mtoto au za *Ntaguye*

Utafiti huu ulibainisha kuwa ujinaishaji wa Wameru uliongozwa kwa kiasi kikubwa na sifa za mtoto aliyezaliwa na vilevile za ntagu yake. Hizi zilikuwa sifa zilizoweza kuonekana au zisizoonekana kama vile za kimapenzi. Sifa hizi pia zingekuwa za mahali, hali, maumbile au vitu alivyokuwa navyo au alivyohusishwa navyo.

**Kirimi -** Shughuli kuu ya Wameru ilikuwa ni kilimo cha mimea kwa ajili ya chakula au mauzo. Mwanaume aliyesifika kwa ukuzaji wa vyakula aliitwa Kirimi au Murimi na mwanamke akaitwa Karimi. Viambishi -ki- na -mu- viliambishwa kwenye vitenzi kuonyesha hali ya kubobea kwenye shughuli hiyo. Jina Kirimi liliashiria apendaye kulima kwa kutambulisha jinsia ya kiume lakini Murimi ingawa lilikuwa la kiume kimaana lingeweza kutumika kurejelea mtu wa jinsia yoyote likimaanisha mkulima.

**Kithinji -** Maana yake ni mchinjaji. Uchinjaji ulifanywa na wanaume kwani wanawake hawakuruhusiwa kuwachinja wanyama katika utamaduni wa Kiafrika na hasa kwa Wameru. Ingawa shughuli hii ingefanywa na mwanaume yeyote, kulikuwa na wale waliotajika katika uchinjaji ambao walitumika kuwachinjia wengine hasa kulipokuwa na sherehe fulani. Kwa hivyo mtoto ambaye *Ntagu* wake alikuwa maarufu kwa uchinjaji angeitwa Kithinji. Hii ndiyo maana hakuna mwanamke angepewa jina Kithinji au Kathinji kwa vile hawakuruhusiwa kufanya shughuli hii. Hii inadhihirisha uwezo ambapo wanaume walichukuliwa kuwa na uwezo kuliko wanawake. Jambo hili lilidhihirisha dhana ya ubaguzi katika majina ambapo mwanamke alibaguliwa kwa msingi ya uwezo na itikadi kwa ambavyo hangeruhusiwa kuchinja ambacho kilikuwa kitendo cha wanaume pekee. Hali hii ilidhihirisha uwezo kiume ambapo mwanaume alipewa mamlaka na majukumu kwa kumbagua mwanamke.

**Mutembei / Mugendi -** Majina haya yalitokana na kitendo cha kutembea au kwenda yatokanayo na mashina ya vitenzi vya Kiswahili tembea na enda. Jina Mugendi au Kagendi lilitokana na kitenzi *enda* ambacho kwa Kimeru asili ni *genda* mzizi -*gend*- ni sawa na Mutembei ambalo latokana na kitenzi *tembea* na mzizi *temb*- ambacho pia humaanisha kwenda. Aliyepewa jina

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

hili inamaanisha alipenda kusafiri. Majina ya kike yaliyo na maana sawa na haya ya kiume ni Kagendo au Kajira ijapokuwa hayamaanishi moja kwa moja hali ya kwenda bali yanamaana kuwa walizaliwa safarini au huwa njiani kila wakati kwa hivyo nao hupenda kusafiri.

**Kinyua au Kanyua** – Lilitokana na kitendo kunywa mzizi wake ukiwa ni –nyw-. Ilimaanisha kuwa mtu aliyepewa jina hilo alipenda tabia ya kunywa vitu kama chai, uji lakini zaidi unywaji wa pombe. Ingawa kuna vitu vingi vilivyonywewa, pombe ndicho kinywaji kilichoashiria tendo hili la unywaji. Siku hizi watu wanaoitwa Kinyua/Kanyua si lazima wawe wanapenda kunywa ila *Ntagu* wao alikuwa anaitwa hivyo kutokana na sifa hiyo ya ulevi au akawa na jina jingine tofauti na Kinyua / Kanyua lakini akawa na tabia ya kulewa kwa hivyo mtoto aliyepewa jina kutokana naye ikambidi aitwe hivyo.

**Makena -** Kwa mujibu wa Wz, hili ni jina la kike ambalo lilimaanisha mtu aliyekuwa na bashasha au tabia ya kufurahi. Lilitokana na *Ntagu* ambaye alikuwa mchangamfu karibu nyakati zote. Yeye hata alipokasirishwa alikuwa hahifadhi hasira bali alionekana mwenye furaha wakati wote. Hili ni jina ambalo lilipendwa sana na kizazi cha sasa. Wasichana wengi waliohojiwa walipenda majina ya kisasa kama Makena na Kendi. Jina lingine la msichana lenye maana sawa na hili ni Kagwiria. Lilimaanisha aliyefurahisha wengine kutokana na tabia zake. Jina hili limeazimwa kutokana na jamii ya Wameru ya kati ambapo katika eneo hilo kitenzi *kugwirua* humaanisha kufurahi lakini kwa Wamwimbi ambapo utafiti huu ulijikita kitenzi sawa na hiki ni *gukena* ambacho ndicho asili ya jina Makena. Mwanamume mwenye sifa ya kufurahi aliitwa Mugwiria kutokana na *kugwirua*. Kutokana na utafiti huu jina Makena au Kagwiria kwa msichana lilitumika sana katika eneo hili lakini Mugwiria la kiume halitumiki sana.

**Kendi -** Jina hili lilimaanisha anayependa. Ilimaanisha kuwa *Ntagu* wa aliyepewa jina hili alikuwa na sifa zilizopendeza watu hivyo wakampenda kwa ambavyo yawezekana alisema na watu vyema, aliwatendea vyema au alikuwa na sura ya kupendeza. Angeweza pia kuwa wa pekee katika familia kama vile kifungua mimba kwa vile wazazi hawakuwa na mwingine wa kupenda kwa hivyo walipompata wakawa wanampenda. Iwapo sifa ya *Ntagu* ingekuwa ya kupenda basi mtoto angeitwa Kendi kumaanisha yeye ndiye alipenda watu. Jina lingine la msichana lililomaanisha kupendwa ni Kiende. Hili kiasili lilitumika sana katika sehemu ya imenti lakini pia likapata kutumika katika sehemu hii ya Mwimbi ingawa kwa uchache. Majina ya kiume yenye sifa hii ya kupenda au kupendwa ni Mwenda na Mwendwa. Ingawa majina haya yalikuwa ya kimajazi utafiti huu ulionyesha kuwa si watu wote walioitwa hivyo waliomiliki sifa hizo za kupenda au kupendwa. Kuna walioitwa Kendi (msichana) Mwenda (mvulana) lakini hawakupenda mithili ya majina yao. Hii ni kwa sababu tabia ya mtu mwingine ilichangia upataji wa jina la mtoto ambaye si lazima angeziiga tabia hizo.

**Kanini -** Humaanisha kitu kidogo. Hili ni jina la mwanamke lenye sifa ya udogo. Jina hili hupewa mtoto iwapo *Ntagu* wake alikuwa mdogo ki maumbile. Ingawa unene ulizingatiwa, kimo cha mtu ndicho kilichangia uamuzi wa kurejelewa kama mdogo au mkubwa. Wembamba na ufupi ulichukuliwa kuwa udogo kwa jumla. Ijapokuwa jina hili lilimaanisha aliyerejelewa alikuwa mdogo, hakupuuzwa kutokana na maumbile haya. Wanaume hawangepewa jina hili kwa sababu ya ubabe dume. Kwa mwanamume hata akiwa ni mdogo bado yeye alionekana sawa na udogo haungempunguzia hadhi kama ilivyokuwa kwa wanawake. Huu ulikuwa ni mkakati wa kuzua ubishi kuhusu ujinaishaji ambapo jinsia ya kike ilibaguliwa na kuonekana kuwa itikadi iliyokubaliwa katika jamii kuwa wanawake wako chini kihadhi wakilinganishwa na wanaume. Mwanaume hata kama alikuwa mdogo aliheshimiwa kutokana na majukumu yake kama mwanamume kwa hivyo hangepewa jina hili.

**Mucheke** – Jina hili humaanisha mwembamba. Huwa la mwanaume. Aliyepewa jina hili ilimaanisha *Ntagu* wake alikuwa na umbo jembamba kwa kulinganishwa na wengine. Kulingana na utafiti huu wembamba ulikashfiwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

kuliko unene ambao ungekuwa kinyume chake kwa vile Wameru hawakujali unene wa mwili kwa kuwa mtu mnene angesifika ilhali mwembamba angeonekana amekosa kitu fulani labda kutokula vizuri au kuwa na shida kama ugonjwa au umaskini. Wembamba huu ulikuwa wa kimaumbile lakini haukutokana na shida au visababishi vingine kama magonjwa. Neno lililotumiwa na Wameru kurejelea hali ya wembamba ambayo ilisababishwa na shida kama magonjwa au njaa ni *Nchengu.* Lilimaanisha mtu aliyekonda. Labda mtu kama huyu alikuwa mnene lakini kwa sababu ya shida akakonda. Jina hili lilitumiwa kama la lakabu kurejelea mtu aliyekuwa mnene lakini akabadilika na kuwa mwembamba. Hili ni jina lililotumika sana miongoni mwa vijana kwa njia ya kutania umbo la mtu.

**Ngai / Kangai** – Ngai ni jina la kiume na Kangai ni la kike. – Yalitokana na sifa ya kimajaaliwa *ya ntagu* yao aliyeitwa hivyo kwani alinusurika wakati akiwa mdogo. Yawezekana aliugua sana na kuponea chupuchupu kuaga dunia. Ilimaanisha alipona kwa majaliwa yake Mungu. Mtoto pia angepewa jina hili iwapo waliozaliwa kabla yake waliaga kwa hivyo ili kuzuia asichukuliwe na mizimu ya waliokufa, alipewa jina la Mungu badala ya la binadamu. Majina haya yalionyesha hali ya kutegemea Mungu aliye na uwezo wakati mambo yanapoharibika.

**Muchunku -** Jina hili humaanisha Mzungu. Wazungu walikuwa tofauti kirangi na kitabia wakilinganishwa na Waafrika. Ingawa wazungu walifukuzwa bado athari zao zazidi kudhihirika kutokana na baadhi ya majina ambayo Waafrika waliwapa watoto wao yaliyokuwa na asili au athari za kikoloni. Jina hili lilitokana moja kwa moja na jina Mzungu lililorejelea mzaliwa wa bara Uropa na mweupe pe! Mtoto aliyepewa jina hili ilimaanisha labda alizaliwa kipindi hicho ambapo Wazungu walifika katika eneo hili la utafiti. Alipewa jina hili kwa ukumbusho wao. Vile vile angepewa jina hili kutokana na Mzungu aliyefika sehemu fulani na kufanya mambo yaliyopendwa na jamii hivyo, jamii hiyo ikachagua jina lake bila hata kumjulisha. Aidha, jina Muchunku lingetokana na hali ambapo *Ntagu* wa mtoto aliiga tabia ya kizungu kama vile kupenda kuongea, kuamrisha, kutunza wakati na kupenda usafi kama vile mzungu. Iwapo mtoto alizaliwa wakati wa majilio ya Wazungu pia angeitwa Muchunku kama kumbukumbu ya tukio hilo. Kwa hivyo hili ni jina la watu waliozaliwa wakati wa ukoloni na baada ya wakoloni kuondoka.

**Ruguru** – Humaanisha magharibi. Huu ni upande ambao jua huchwa wakati wa jioni. Katika eneo hili la utafiti upande huu huashiriwa na mlima Kenya. Neno hili hutumiwa katika muktadha mwingine kurejelea sehemu iliyo magharibi mwa mahali ambapo mtu yupo. Wameru pia hurejelea watu wa magharibi mwa Kenya kama "*antu ba ruguru"* watu wa upande wa juu au magharibi kwa sababu kulingana na dira wao wako upande wa magharibi mwa Kenya. Kutokana na hali hii, *ruguru* ni tofauti na *iguru* kwa ambavyo *Ruguru* ni magharibi na *iguru* ni juu lakini *Ruguru* linaweza kutumika kwa maana ya upande au juu kutegemea muktadha. Mtoto alipewa jina hili iwapo ntaguye aliishi upande wa juu au aliolewa kutoka upande huo.

**Umotho -** Lilimaanisha upande wa kushoto. Kushoto ni upande ambao moyo wa binadamu huwa nao kulia ni ulio kinyume chake. Wameru wanathamini sana upande wa kulia kwa sababu hata watu wengi hutumia mkono na mguu wa kulia kufanyia kazi kama kuandika, kukatia au kupigia. Wa kushoto haufanyi kazi vyema isipokuwa kwa watu wachache tu nao hudhihakiwa na wengine wasioutumia. Katika eneo la Mwimbi upande wa kushoto hutambuliwa kwa kuelekea au kukabili mji wa Meru nao wa kulia kuelekea mji wa Chuka. Watu ambao huitwa Umotho humaanisha *Ntagu* yao aliishi upande wa kushoto au alienda na kukaa huko kabla ya kurejelea kwao na wakati huo mtoto aliyepewa jina kutokana naye akazaliwa. Ni kinaya kuwa Wameru walitumia jina Umotho - upande ambao haukuthaminiwa sana kupata majina ya watoto badala ya wa kulia uliothaminiwa.

**M'Nyiri** - Hili ni jina ambalo mwanaume alipewa kutokana na tabia yake ya kwenda mjini

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

Nyeri kwa ajili ya biashara au kutafuta kazi. *Nyiri* katika matamshi ya Kimeru ni mji mkuu wa jimbo la Nyeri uliokuwa makao makuu ya mkoa wa kati. Kiambishi 'M' kinachotangulia jina la mji huu huashiria binadamu anayehusishwa na mji huo. Mtoto ambaye alipewa jina kutokana na *Ntagu* aliyekuwa akienda Nyeri kwa ajili ya biashara au kazi angeitwa M'Nyiri. Jina hili pia lingetokana na ndege aliyeitwa Kanyiri kwa kupenda kuringa na kutikisha mbawa zake za nyuma kwa hivyo kama mtu alikuwa na tabia kama za ndege huyo angepewa jina M'Nyiri.

**M'Ragwa** – Jina hili lilitokana na mahali palipoitwa Maragwa ambao ni mji ulio baina ya Murang'a na Sabasaba. Jina hili lilipewa mtu ambaye alikuwa miongoni mwa vijana walioenda Maragwa kutafuta kibarua au walitua katika mji huo wakielekea mjini Nairobi kwa madhumuni ya kutafuta kazi. Wanaojulikana kwa jina hili leo inamaanisha kuwa *Ntagu* zao walishiriki safari hizo na wakapewa jina hilo ili kuwakilisha wengine. Siku hizi wanadondoa kiambishi 'M' ili yasikike ya kisasa. Mifano ya majina yaliyotokana na sifa hii ni M'Nairobi aliyeende Mjini Nairobi, M'Thika aliyeenda Mjini Thika, M'Muranga aliyeenda Mjini Muranga na M'Miiru aliyeenda mjini Meru. Aidha, M' Ngonyi alienda mahali palipoitwa Ngonyi (kabla ya kufika mjini Meru).

Kutokana na maoni ya Wz, ilibainika kuwa tabia ya *Ntaguye* mtoto iwe chanya au hasi ilichangia pakubwa upataji wa jina la mtoto. Vilevile walieleza kuwa Wameru walitazamia kuwa mtoto angemiliki sifa na tabia za *Ntagu* yake. Aidha, wazee hao ndio tu walitaja jinsi sifa ya kiushujaa na kimaumbile zilivyochangia ujinaishaji kwa aliyezidhihirisha. Mawazo haya hayakuelezwa na mhojiwa yeyote kutoka katika makundi ya vijana, kuonyesha kuwa wazee ndio tu walielewa kwa undani mfumo huu wa ujinaishaji.

**Ujinaishaji kutokana na majina ya ukoo.**

Kulingana na kisasili cha Wameru, walitoka mbwaa (pwani) mahali ambapo palikuwa kitovu chao miaka mingi iliyopita.Wazee hao walieleza kuwa waliohama walifika katika maeneo wanamoishi kwa awamu tatu kulingana na majira ya siku. Kundi la kwanza lilifika usiku kukiwa na giza. Hawa waliitwa Njiru (kumaanisha weusi yaani giza). Kundi la pili nalo likawasili likifuatia wakati wa mapambazuko waliitwa Ntune (kumaanisha wekundu wa kupambazuka) Kundi la tatu lilifika mchana jua likiwa linawaka nalo likaitwa Njeru (kumaanisha mwangaza wa jua waliloita *Njeru*) kwani jua ndilo lilileta *Weru* (mwangaza). Makundi haya matatu ndiyo yalikuwa *Miiriga* (koo) asili za Wameru na nyingine zilitokana na koo hizi tatu. Kila mtu hujitambulisha kwa ukoo fulani.

**Mukwanjeru** – Jina hili lilipewa mtoto ambaye *Ntagu*ye aliolewa na mume aitwaje Njeru kutokana na ukoo asili wa Njeru waliofika mchana kukiwa na mwangaza wa jua. Jina hili pia lilitumiwa na wanawake wa makamo waliozaliwa hadi kufikia miaka ya sitini. Watoto wanaozaliwa siku hizi hawapewi jina hili kwani lachukuliwa kuwa la kale lililopitwa na wakati.

**Mukwanjiru** - Hili lilitokana na ukoo (*mwiriga)* wa Airu ambao walitoka katika ukoo asilia wa Njiru. Lilipewa mtoto aliyekuwa na *Ntagu* aliyeolewa na mume wa ukoo wa Airu. Jina hili pia ni la kizamani na halikujinaishwa watoto wa sasa bali lilithaminiwa sana na wazee ambao walielewa maana yake.

Utafiti ulibainisha kuwa ingawa kuna watu walio na majina haya ya ukoo wengi hawakujua maana yake hasa vijana na baadhi ya wanawake wa makamo. Wazee wote waliohojiwa walijua maana yake na waliyapenda kwani yalionyesha asili ya Wameru. Kulingana nao mfumo huu wa kutumia majina ya kiukoo unazingatiwa na makabila mengine kama Wakikuyu walio na majina kama Wanjiru–ukoo wa Njiru, Waithira –ukoo wa Mathiru ambayo yalitokana na *koo(miiriga)* ya kwanza tatu (Njiru, Ntune na Njeru).

**Mfumo wa kutumia majina ya Nyoni**

Kwa mujibu wa wazee wanne wa kiume na mmoja wa kike, *Nyoni* ilikuwa ni namna ya utambulisho wa mtu binafsi *kutokana* na ukoo wake ambao asili yake ni zile koo tatu za kiasili za

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

Wameru. Kila mtu huwa na *nyoni* yake anayotambulishwa kwayo. Yapo majina ya kike na ya kiume yaliyotokana na *Nyoni* mathalani:

**Mukwanjue** - Ni jina la kike. Lilimaanisha *Ntagu* wa Mtoto alikuwa wa *Nyoni* ya Njue. La kiume lilikuwa Njue. Siku hizi halitumiwi kwa wasichana ila kwa wanawake wakongwe lakini kwa vijana lingali katika matumizi ingawa kwa uchache.

**Mukwadadi** -Jina hili pia ni la *Nyoni* ambalo mtoto alipewa kutokana na *Nyoni* ya *Ntagu*ye. Kati ya wazee wote na vijana waliohojiwa hakukuwa na yeyote aliyepewa jina hili. Ilibainika kuwa jina hili halitumiwi siku hizi kutokana na mtazamo wa watu kuwa ni la kale na pia kutoelewa maana yake. Kuna majina mengi ya *Nyoni* hasa ya kiume kama vile; Ireri, Ntwiga, Njeru, Njagi na Nyaga ambayo yanatumiwa hadi sasa na vijana wakubwa.

**Mfumo wa kutumia majina ya Rika (*nduki)***

Utafiti huu ulibainisha kuwa Wameru walijinaisha kutokana na majina ya nduki (Rika). Kulingana na wazee wanne wa kiume, *nduki* au Rika ni ruwaza ya kutambulisha umri wa watu kulingana na nyakati mbalimbali za upashwaji tohara. Kwa mujibu wa wazee hao upashwaji tohara ulifanyika mara moja kwa mwaka au baada ya miaka mitatu kutegemea ukomavu wa vijana ambao wangetahiriwa. Nduki moja ilijumuisha wapashwa tohara wa awamu tatu kila moja ikiwa na jina lake la kujitambulisha na kisha kuchukua jina la nduki mojawapo hasa ya kwanza ili kusimamia zingine. Kwa mfano, nduki ya Kathenya, Mbae na Kibabu ziliitwa Kibabu. Kulingana na utafiti huu majina ya nduki yalipewa watu waliokuwa na majina yao ya kwanza lakini wakati mwingine hayo ya rika yalizoewa na kutumika kwa utambulisho wa mtu. Majina hayo yalirefushwa kwa kuambishwa kiambishi -M- ili kupata ya kiume na kiambishi –Ji- kupata ya kike. Mfumo huu wa majina ulitumiwa kwa wanaume walipotahiriwa na wanawake walipoolewa. Mabadiliko haya ya majina yalikuwa namna ya kuonyesha heshima kwa kuvuka hatua muhimu ya maisha.

**Ragu** – Kulingana na Mzm 1 – 2, jina hili lilikuwa la rika ya zamani sana kadri ya uwezo wao wa kukumbuka. Kulingana nao, rika hili lilikuwa mnamo mwaka wa elfu moja na mia saba. Rika hili lilifuatwa na rika la Kibabu ambalo baadaye lilifuatiwa na rika la Kubai. Haya hayakuwa ndiyo marika kongwe zaidi bali kuna mengine yaliyotangulia lakini hayakujulikana na wahojiwa. Kutokana na marika haya kuna majina ya kiume kama M'Mbaabu, M'Kubai na M'Kaburia. Majina ya kike yaliyotokana na marika hayo yalikuwa kama Jiambabu, Jiakubai na Jiakaburia au Jiamburia. Kulingana na wahojiwa wazee, mfumo huu wa kujinaisha kulingana na marika ulikuwa mzuri kwani ulionyesha tofauti za kiumri za watu mbali mbali. Kulingana nao ilikuwa njia bora ya kukumbusha wakati mtu alizaliwa na vilevile matukio makuu yaliyotokea nyakati tofauti katika historia. Waliridhishwa na matumizi ya viambishi 'm' na 'ji' Katika majina kwani vilionyesha heshima na kuwatofautisha na vijana ambao hawakuwa wamepashwa tohara au kuolewa.

**Kaburia** – Hili ni jina lililopewa rika ambalo lilifuata rika la Ragu. Lilijumuisha rika tatu zilizojulikana kwa majina tofauti kama Kaburia ambalo lilitangulia kutahiriwa, Kamundi na kufungiwa na Kabae. Ingawa rika la Kabae ndilo lilimalizia awamu hizo tatu, jina lake linajulikana sana kwa vile wazee na vijana wengi wanaitwa Mbae kumaanisha walipewa majina kutokana na rika hilo. Kutokana na majina hayo ya rika ndipo majina yatumiwayo sasa yalipopatikana. Kwa mfano, M'Kabae, M'Kaburia na M'Kamundi. Utafiti huu uliweza kubainisha matumizi ya majina haya kwa wazee na vijana wa sasa. Wazee wote walijua asili na maana ya majina yao lakini vijana hawakujua. Wanawake walipewa majina haya lakini yaliambishwa kiambishi -ji- mwanzoni. Kulikuwa na majina kama Jiambae, Jiakaburia na Jiamundi yote yakiashiria rika lake. Siku hizi majina haya hayatumiwi kwa watoto kwa kuwa kizazi cha sasa hakijui mfumo huo wa rika na hakiupendi kwani ni wa kale na uliopitwa na wakati.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

Kutokana na mifano hii, ilidhihirika kuwa licha ya kuwa na mfumo wa kujinaisha kutegemea sifa ya mtu, Wameru walikuwa na mifumo mingine mitatu ya ujinaishaji.Wazee wengi waliielewa yote lakini wachache tu ndio hawakuelewa kama vile mfumo wa kutumia *Nyoni*, Rika na Ukoo.

**Hitimisho**

Kwa muhtasari, utafiti huu ulibainisha kuwa Wameru huwa na mifumo mahsusi ya ujinaishaji iliyoongozwa na vipegele vifuatavyo: Sifabia za mtoto au za *Ntagu*ye kama: kazi aliyofanya, sifa za kidhahania, maumbile ya mwili, matendo aliyopenda, mahali pa kuzaliwa, majira na hali ya mtoto aliyezaliwa na vilevile sifa za kishujaa. Majina pia yalitokana na sifa za kisitiari kama: Matukio makuu ya kihistoria, majina ya pande za dira, na majina ya mahali na miji maalum. Ujinaishaji pia ulichangiwa na ruwaza za kijamii kama: Majina ya Ukoo, majina ya *Nyoni*, na majina ya Rika.

**Mapendekezo**

Utafiti huu ulishughulikia mifumo ya ujinaishaji ya Wameru kwa kuegemea semantiki ya majina. Inapendekezwa watafiti wengine washughulikie suala la mofolojia na fonolojia ya majina katika jamii hii.

**Faharasa**

***Ntagu*** **:** Jina la mtu ambaye mtoto hupewa jina kutokana naye

***Nyoni*** **:** Jina la utambulisho ambalo mtu hujipa na hurithiwa na mtoto ambaye hujinaishwa kutokana naye.

**MAREJELEO**


Abate Fr, Ed. (1994). *Proper Names Master Index, A comprehensive index of proper names* Detroit.

Abagi, M. (1995*). An Anthropology of Names and Naming*. Cabridge.Cabridge University press.

Aswani, Mayaka na Riro (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Serengeti Publishers. Mwanza.

Barnes R. H, (1980). 'Hidasta personal names': *An Interpretation Plains Anthropologistics Journal of anthropological Research* /25 90311-31281.

Berly, A. (2013*).*'African Naming Practices': *Journal of pan Africa studies Vol. 7 no.8/7* South Carolina.

Beidelman, B. (1974). *An Alphabetical Guide to the Language of Name Studies Lanham and London, The Scarecrow* Press.

Buren, D .V (1977), *English personal names, Retrived from* https // books. Google.com 15th April, 2017.

Edward, S. (1996), *Journal of Languages and Culture. Personal Name and history*. Retrived from http://www.journals. Org /.../... on 10th March, 2017.

Garry,T.(2000). *Ethinic Naming Customs*. Retrieved from http://www.scn.sap.babynames.co on 2nd February, 2017.

Greg, C. (2014), Retrived from https://www. baby *centre. Com- names*…, *Social science space*. com, Sage publications on 15th January, 2017.

Greenberg, S. (1980) *African Names: Names from the Africa Continent for Children and Adults.* Newyork.

Good, C.U. (1963), *Introduction to Education Research*, New York, Appleton Century Croft

Idowu, E.B. (1991*). Introduction to tradition Religion* SCM press, London.

Laura, A. ( 2009), *The Oxford Hand book of Names and Naming.* Oxford University press United Kingdom.

Mugambi, J.N (1989), *African Heritage and Contemporary Christianity.* Longman, Nairobi, Kenya.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2100

Mbiti, J.S (1992) 2nd Ed. *African Religious and Philosophy* Heinemmann, London.

Mugenda, O and Mugenda, A. (1999), *Research Methods Qualitative and Quantitative*

*Approaches*, Nairobi, African Center for Technology Studies (Acts) Press

Onyango, G.A. (2001), *Competencies Needed by Secondary School Head Teachers and*

*Implications for Pre-Service and In-Service Education,* A Case Study of Nairobi and Kakamega District (Kenya), Unpublished PhD. Thesis, Kenyatta University

Orodho, A. J. (2003). *Elements of Education and Social Science Research Methods*. *Nairobi:* Mazola Publishers.

Pamela, R. And Linda, R (2004), *Cool names for Babies*: Retrived from htttp: //www.amazon. com /... Names... on 7th April, 2017.

Webber, M. (1987). 'Ethics as Personal Names'Greek Personal Names.Their values as Evidence. Oxford University Press.

Wierzbicker, A. (1992). *Semantics Culture And Cognition Universal Human Concepts In*

*Culture Specific Configurations.* Oxford university press. New york.

The New Constitution of Kenya (2010), Government printer, Nairobi, Kenya.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.